# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI MAKAMBAKO - MAKUWASA

## TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA MAJI BWAWANI KWA KAMATI YA SIASA YA WILAYA

Serikali inatekeleza Mradi wa kuboresha huduma ya maji mjini Makambako kwa kujenga mradi wa maji Bwawani. Mradi huu unatekelezwa kwa mgawanyo wa mkandarasi mmoja na wazabuni wawili ambao ni **Pipes Industry Ltd., S.L.P 16541 Dar es Salaaam** anayeleta mabomba yenye kipenyo cha inchi 3 kwa gharama ya Tsh. **161,673,620.00**, **NAJJA Hardware, S.L.P 6398 Dar es Salaam** anayeleta viungio vya mabomba kwa gharama ya Tsh. **61,395,400.00** na mkandarasi **Building, Water and Earth Works Ltd., S.L.P 62059 Dar es salaam** anayejenga mradi kwa gharama Tsh. **1,568,669,761.00**.

Mradi huu unatekelezwa kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kuanzia tarehe 08/06/2017 siku ambayo mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi. Mradi huu unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa **(IRUWASA)** kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako **(MAKUWASA)**.

**Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi huu ni;-**

- Ujenzi wa mtego wa maji (intake) wenye uwezo wa kuzalisha lita 336,000 kwa siku na kuimarisha bwawa.

- Ujenzi wa tanki la chini (SUMP TANK) lenye ujazo wa lita laki moja (100,000).
- Ulazaji wa bomba la inchi 6 toka kwenye chanzo cha maji (Intake) kwenda kwenye tanki la chini la lita 100,000 kwa umbali wa mita 92.
- Ujenzi wa kibanda cha mitambo na cha mlinzi.
- Ufungaji wa umeme kwenye nyumba ya mitambo (HT line).
- Ununuzi na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji zenye uwezo wa kusukuma lita 14,000 kwa saa kila moja.
- Usafishaji wa visima viwili vilivyopo katika eneo la chanzo na kuviunganisha kwenye tanki la lita laki moja kwa umbali wa mita 160.
- Ujenzi wa uzio kuzunguka chanzo cha maji kwa umbali wa mita 1000.
- Uchimbaji wa mtaro, ulazaji wa bomba na ufukiaji wa mita 1,970 kutoka Bwawani mpaka litakapojengwa tenki.
- Ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita laki tano (500,000) na urefu wa mita kumi na mbili (12) kwenda juu.
- Umaliziaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi.
- Ujenzi wa uzio wa kuzunguka Ofisi kwa umbali wa mita 260.5
- Ununuzi wa samani za Ofisi.

**Kazi zilizofanyika mpaka Disemba 31, 2019 ni kama zifuatavyo:-**

- Uletaji wa mambomba umekamilika kwa 100%.
- Uletaji wa viungio vya mabomba umekamilika kwa 90%.

- Ujenzi wa mtego wa maji (intake) wenye uwezo wa kuzalisha lita 336,000 kwa siku na kuimarisha bwawa umekamilika kwa 100%
- Ujenzi wa tanki la chini lenye ujazo wa lita laki moja (100,000) umekamilika kwa 100%.
- Ulazaji wa bomba la inchi 6 toka kwenye chanzo cha maji (Intake) kwenda kwenye tanki la chini la lita 100,000 kwa umbali wa mita 92. Kazi hii imekamilika kwa 100%.
- Ujenzi wa kibanda cha mitambo na cha mlinzi umekamilika kwa 80%.
- Ufungaji wa umeme wa njia kuu (HT Line) imekamilika kwa 100%.
- Ununuzi na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji zenye uwezo wa kusukuma lita 14,000 kwa saa kila moj Kazi hii imekamilika kwa 100%
- Usafishaji wa visima viwili vilivyopo katika eneo la chanzo na kuviunganisha kwenye tanki la lita laki moja kwa umbali wa m ita 160. Kazi hii bado haijaanza.
- Ujenzi wa uzio kuzunguka chanzo cha maji kwa umbali wa mita 1,000. Kazi hii imefanyika kwa asilimia 75%
- Uchimbaji wa mtaro, ulazaji wa bomba na ufukiaji wa mita 1,970 kutoka Bwawani mpaka litakapojengwa tenki umekamilika kwa 100%
- Ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita laki tano (500,000) na urefu wa mita kumi na mbili (12) kwenda juu umekamilika kwa 80%.
- Ujenzi wa jengo la Ofisi umekamilika kwa 75%.

- Ujenzi wa uzio wa kuzunguka Ofisi kwa umbali wa mita 260.5 umekamilika kwa 78%.
- Ununuzi wa samani za Ofisi. Kazi hii bado haijaanza.

Mpaka Disemba 31 ,2019 kwa ujumla mradi umefikia wastani wa 75% ya ujenzi. Mpaka Septemba, 2018 mkandarasi ameshalipwa jumla ya kiasi cha **Tshs. 485,027,989.00**

**Changamoto**

1. Changamoto iliyopo katika mradi huu ni kuchelewa kwa kukamilika kwa ujenzi wa mradi kwa mujibu wa mkataba. Mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 07/06/2018. Changamoto hii imetokana na Makandarasi kutolipwa madai yake kwa wakati.

2. Pia changamoto nyingine ni uwezo mdogo wa kifedha kwa Mkandarasi. Kutokana na changamoto mbalimbali imelazimika kumuongezea mkandarasi muda wa kutekeleza ujenzi wa mradi hadi tarehe 08/02/2019 lakini mpaka sasa bado hajakamilisha ujenzi.Hali hii ililazimika kumuongezea tena muda wa ziada ambao utamalizika tarehe 28/02/2020.

3. Mifereji ya maji machafu/ya mvua iliyojengwa na kuelekezwa kwenye chanzo cha maji cha bwawani hali ambayo inasababisha uchafuzi wa chanzo hasa kipindi cha masika na kupelekea maji kutokusukumwa kupelekwa kwa Wananchi kwa ajili ya matumizi

**Hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto hizo**.

- Timu ya Wataalamu imeainisha shughuli muhimu ambazo alielekezwa Mkandarasi azitekeleze ili mradi uanze kutoa huduma ifikapo tarehe 30/10/2018 wakati shughuli nyingine zilizobaki zikiendelea kutekelezwa. Utekelezaji wake ulifanyika na huduma kipindi cha kiangazi iliweza kupatikana.

- Kuhusu mifereji ya maji machafu iliyojengwa kuelekea kwenye chanzo cha Maji cha Bwawani, tayari jitihada zimefanyika ikiwa ni kukaa vikao baina ya TARURA, Halmashauri ya Mji, na Mhe. Mkuu wa Wilaya na kukubaliana kila Taasisi ichangie kiasi cha fedha ili kurekebisha mifereji hiyo. Pia MAKUWASA tumeandika barua Wizara ya Maji kuomba fedha kwa ajili ya kuhamisha mifereji ya maji machafu. Taratibu za upatikanaji wa fedha hiyo zinaendelea.

**Matarajio baada ya kukamilika mradi**

Matarajio baada ya kukamilika kwa mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa maji wa lita **336,000** kwa siku ambao utaongeza idadi ya watu wapatao huduma ya maji kwa wastani wa **5.1%.** Hii ni sawa na wakazi **4,800** ambao watanufaika na mradi huu. Aidha, mradi huu ukikamilika huduma ya maji itaongezeka toka **58.9%** ya sasa hadi kufikia **64%.**

Naomba kuwasilisha,


Eng. Lufyagile, *O. A*

**Kaimu Mkurugenzi**

**Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Makambako**